kutokana na hilo, aliwataka madiwani kuendelea kuisimamia menejimenti ili hoja zote zipatiwe majibu ya kuridhisha na

Igunga, Lucas Bugota, aliwataka watumishi wa halmashauri hiyo kuendelea kuchapa kazi na kuzifuatilia hoja zote zilizobaki.

UHURU UK 5.

# *Wafugaji waelezwa faida za kuogesha mifugo yao*

**Na LILIAN JOEL**, *Arusha*

WAFUGAJI wa Halmashauri ya Arusha, Wilaya ya Arumeru, mkoani hapa, wametakiwa kuogesha mifugo yao, ili kuiepusha na magonjwa yanayosababisha idhoofike na wakati mwingine kufa.

Ushauri huo ulitolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Seleman Msumi, mwishoni mwa wiki, alipokuwa akizindua josho la kanda C, lililofanyiwa ukarabati na wafugaji wa Kijiji cha Lemanda, Kata ya Oldonyosambu.

Wafugaji hao walifanya hivyo, baada ya serikali kuanzisha mkakati wa kutoa dawa za kuogeshea mifugo katika maeneo mbalimbali nchini.

Msumi alisema serikali inatoa ruzuku ya fedha nyingi za dawa za kuogesha mifugo, lengo kuhakikisha inakuwa salama.

"Hivi sasa josho hili linafanya kazi, niwatake wafugaji wote katika Halmashauri ya Arusha kuogesha mifugo yao kila mara kwa mujibu wa utararibu watakaopatiwa na wataalamu wa mifugo, ili kuepuka magonjwa hatari yanayoidhoofisha na wakati mwingine kusababisha kufa," alisema.

Alisema kuna magonjwa mengi yanayoenezwa na wadudu aina ya kupe na ndorobo yanayoua mifugo kwa asilimia 70 hadi 100 na kusababisha uchumi wa wafugaji na familia zao kuyumba.

Msumi aliwapongeza wafugaji hao kwa kukarabati josho hilo la kuogesha mifugo na kuwataka kuendelea kulitunza.

Wafugaji wa Lemanda, waliishukuru serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa kuwapatia ruzuku ya dawa ya kuogeshea mifugo, zilizowapa hamasa ya kukarabati josho hilo lililosimama kutumika kwa zaidi ya miaka 20, kwa kushindwa kujiendesha.

Mwenyekiti wa kamati ya kusimamia uendeshaji wa josho hilo, Peter Leskari, aliahidi litakuwa mwarobaini wa magonjwa ya mifugo yanayosababishwa na wadudu na litarejesha matumaini mapya kwa wafugaji kwa sababu awali baadhi yao walikuwa wakitumia mabomba na wengine kutoogesha kabisa.

Ofisa Mifugo Halmashauri ya Arusha, Omary Sembe, alisema serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inatekeleza mkakati wa kuboresha sekta ya mifugo na wafugaji, kwa kutoa dawa za kuogeshea mifugo bure, ili kuzuia vifo vinavyotokana na magonjwa ya kupe na ndorobo.

Kwa mujibu wa Sembe, magonjwa hayo yanaua mifugo kwa zaidi ya asilimia 90.

"Dawa hii ya kuogeshea mifugo, ina uwezo wa kuikinga kwa zaidi ya asilimia 70 na magonjwa yanayotokana na kupe, ndorobo, ndigana kali, ndigana baridi, moyo kujaa maji. Hivyo, mwarobaini wake ni kuogesha mifugo," alisema.

CamScanner

haya," alisema Rais Samia.

na kuitaka Zanzibar iangalie

nije kufungua," alisema Rais

vijana kiuchumi, kujenga

HABARI LEO UK 2




Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (wa pili kulia) na Kiongozi wa Mradi Lishe Endelevu wa USAID, Dk Joyce Kaganda (kulia) wakionesha miongozo mipya ya ufugaji wa kuku, sungura na samaki baada ya kuzindua mkoani Dodoma mwishoni mwa wiki. Wengine ni wawakilishi wa makatibu wakuu wa mifugo na uvuvi. (Na Mpigapicha Wetu)

MWANANCHI UK 6.

# Kamati ya Bunge yaitaka NAIC kuelimisha wafugaji

Teddy Kilanga, Mwananchi
tkilanga@mwananchi.co.tz

**Arusha.** Kamati ya Bunge ya kilimo, mifugo na maji imekiagiza Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji wa Mifugo (NAIC) kutoa elimu ya faida za kufanya kazi hiyo ili kupata mifugo na mazao yake yaliyo bora.

Akizungumza mkoani Arusha jana, Mwenyekiti wa kamati hiyo Dk Christin Ishengoma alisema mafunzo ya teknolojia hiyo yanapaswa kuwafikia wakulima huko walio.

"Tumeona kwanzia ukusanyaji wa mbegu na jinsi zinavyofanyiwa vipimo lakini pia tumeelezwa kila dume na aina ya mbegu yake na sasa kinachotakiwa ni elimu na ushawishi ili waweze kuitikia jambo hili," alisema Dk Ishengoma katika ziara yake ya kutembelea kituo cha uhamilishaji pamoja na wakala wa mafunzo ya mifugo (Lita), kampasi ya Tengeru.

Akiwa katika ziara hiyo, Mbunge wa Moshi Vijiji ni, Profesa Patrick Ndakidemi alisema hali ni mbaya kwa wafugaji katika majimbo yao, hivyo kwa mbegu walizoziona katika kituo hicho ni vema wagani wakawafikia wafugaji kuwaelimisha.

"Kuna maeneo mengine ambayo hawataamini kuwa tuna kituo kikubwa hivi ambacho kinaweza kutoa huduma nchi nzima, kwa hiyo namuombe waziri na timu yake ya wataalamu kuboresha shughuli za ugani juu ya uhamilishaji ili iweze kuwafikia wafugaji," alisema.

**3,800**

**Wataalamu wa mifugo waliopo nchini kwamujibu wa Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (Liti).**

**17,400**

**Idadi ya wataalamu wa mifugo wanaohitaji nchini.**

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alisema wizara hiyo kwa sasa ina mpango wa kuwafikia wajasiriamali wa mifugo na uvuvi lakini pia kwenda kuzungumza na wafugaji ili waipokee teknolojia hiyo.

"Pia tutaviongezea vituo hivi nguvu ili kuboresha zaidi kwa sababu vimechoka, lakini pia kuendelea kufanya tafiti za kina ili kupata matokeo mazuri zaidi kulingana na aina ya ng'ombe, lengo likiwa ni kuboresha mifugo yetu hapa nchini na kuinua vipato vya wafugaji," alisema Ulega.

Awali, akisoma taarifa yake, Kaimu mkurugenzi mtendaji wa NAIC, Dk Dafay Bura alisema lengo la kuanzishwa kwa huduma ya uhamilishaji ni kusambaza mbegu bora zitakazoweza kuongeza uzalishaji wa nyama na maziwa.

"Uhamilishaji huu una faida nyingi, mojawapo ni kuzuia kuenea kwa magonjwa ya vizazi, kuzuia gharama za kutunza madume, kuepukana na hatari za kujeruhiwa na kupata ndama wengi kutoka kwa dume bora," alisema Dk Bura.

Mtendaji wa Lita, Dk Pius Mwambele alisema kuwa chuo hicho kina wajibu wa kuchangia upatikanaji wa wataalamu wa mifugo nchini, kwani waliopo ni 3800 huku mahitaji yakiwa ni 17,400.

NIPASHE UK 15.

# Vitabu miongozo ya ufugaji vyazinduliwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amezindua vitabu vya miongozo ya ufugaji wa kuku, sungura na ukuzaji wa viumbe maji itakayosaidia wafugaji kufuga kisasa na kukuza kipato ili kujikwamua kiuchumi.

Uzinduzi huo umefanyika jana kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wafadhili wa mradi wa USAID/Lishe Endelevu.

Ndaki, alisema ufugaji wa kuku, sungura na ukuzaji wa viumbe maji ni muhimu kwa taifa, kwa sababu ni shughuli ya kiuchumi kwa ukanda wa Afrika kutokana na kuwa na tija katika kukuza kipato, kutengeneza ajira na kuboresha lishe ya wananchi.

Alisema ufugaji wa kuku ni njia mojawapo ya Watanzania kujitoa kwenye lindi la umaskini, kwa mujibu wa Sensa ya 2012 kuna wafugaji zaidi ya milioni nne wanaofuga kuku kuanzia 10 na kuendelea, ambayo ni sawa na asilimia 55.3 ya wafugaji wote.

"Ufugaji wa kuku, sungura na ukuzaji wa viumbe maji ni shughuli muhimu sana kwasasa katika nchi yetu na kwa uchumi wa wananchi wetu," alisema Ndaki.

"Wananchi wengi wanategemea ufugaji wa kuku ambao umezoeleka na kuku hao wanafugwa na kila mtu tofauti na nyuma watu walidhani ufugaji wa kuku unawahusu kinamama pekee," alisema.

Alisema ufugaji wa kuku na sungura ni njia mojawapo ya kuwatoa wananchi katika hali ya umaskini hasa waishio vijijini, uzinduzi wa miongozo hiyo umekuja wakati muafaka na kuitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kujipanga vyema kuisambaza katika kila ngazi kuanzia halmashauri hadi kata ili iweze kuwafikia walengwa.

"Tunatakiwa kuona ni namna gani tutahamasisha wafugaji ambao ni wanachi wetu ili waingie kwa nguvu kwenye ufugaji wa sungura kwa sababu ni chanzo cha lishe, lakini pia ni chanzo cha kipato kizuri," alisema Ndaki.

Hata hivyo, alisema wizara ikipata fedha katika mwaka ujao wa fedha watahakikisha wanalipa kipaumbele suala la ukuzaji wa viumbe maji.

Alisema tusiwe na hii miongozo halafu ikakaa kwetu tukabaki kuandika taarifa kwamba tumetengezeza miongozo kwa kushirikiana na wadau, lakini ipo kwenye makabati kinachotakiwa ni kuisambaza ili ikalete tija kwa wafugaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya USAID/ Lishe Endelevu, Dk. Joyceline Kaganda, alisema mradi huo ni wa miaka mitano unaofadhiliwa na USAID kwa msaada mkubwa wa watu wa Marekani, na kutekelezwa na Save the Children International na washiriki wake.

Alisema mradi huo unatekelezwa katika mikoa minne ya Dodoma, Morogoro, Iringa na Rukwa na ulianza Oktoba 2018 hadi Septemba 2023.



NEWS

# 0,000 dropouts in education


DAILY NEWS page 4

em ac-
do not
writing
he one
critical
solving

at they
nformal
tion to
hem to
citizens
itude to
of the

rted ef-
social
nd chil-

SQ009088




*MINISTER for Livestock and Fisheries, Mr Mashimba Ndaki (centre) hands over the poultry production guideline to Dr Charles Mhina on behalf of the Permanent Secretary of the Livestock Sector in the docket in Dodoma over the weekend. Right is the Chief of Party for the USAID Lishe Endelevu project, Dr Joyce Kaganda that supported the preparation of the guidelines. (Photo by Ben Bago)*

## Role of cooperatives

## NGO pushes for more youths engagement in economy

**From DAILY NEWS Reporter in Dodoma**

A NON-GOVERNMENTAL Organisation – Tanzania Men as Equal Partners in Development (TMEPID) has called

**"Through the smart advocacy, we have managed to reach a number of them through the Council**